

Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Kuishi na kufa na baadaye kuendelea kuishi.

Kila mtu hukabiliana na kifo chake mwenyewe

(Kitabu hiki kinapatikana katika lugha ya kiingereza)

First Edition in Swahili: October 2021
1ère édition en Swahili: Octobre 2021

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:
Sie leben ewig – es gibt keinen Tod

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Mauti ni kama usiku au giza kwa nafsi. Kufa ukitazama uzima wa milele, ni kama nuru au mchana wa milele kwa nafsi.

Kwa nini watu wengi wana woga wa jambo linaloitwa kifo? Kwa nini watu wana hofu mwingi, woga na kukosa ukubali wa jambo linaloambatana na maisha yetu ya kibinadamu? Dhana ya watu kuhusu kifo inayowatia hofu, wasiwasi au tena kukata tamaa ni dhana potovu na bila uhalisia, ni alama ya upuuzi na kukataa kuelewa kwao, yaani ni madhara ya uhusiano wao na maisha potovu. Sababu za woga huo ni zipi?

Ikiwa kufa kunasababisha hofu kubwa kwa baadhi ya watu ni kwa sababu hawana ujuzi halisi wa ulimwengu, hawatambui nguvu ya ulimwenguni pote isiyoweza kutoweka na wala hawaoni mbali ya uzima wa kimwili.

Uzima hauwezi kukoma. Uzima ni mtiririko wa nuru unaoendelea, mtiririko wa nguvu za kimungu unaotiririka bila kikomo. Hakuna nguvu inayopotea.

Tendo la kuzaliwa duniani linahusiana na lile ambalo tunaliita kifo kwani maisha ya kila mwanadamu ina mwisho wake. Basi kufa ni jambo la asili na la kawaida kama vile kuzaliwa.

Yule anayekataa mwito wa Mungu, anayekataa uzima, hukataa nuru. Anajipatia maskani katika ufalme wa giza, katika ujinga wa kiroho, katika ulimwengu dhahania. Hahisi tena uzima kama jinsi ulivyo, yeye ni kipofu yaani mtu aliyekufa kiroho. Basi mauti ni giza ya nafsi. Kuona kwamba baadhi ya watu huchukua kifo kama hatima ya uzima, hapa chini duniani, kuna wafu wengi wa kiroho na ahera kuna nafsi nyingi sana zilizokufa kiroho.

Yote tunayoyafanya na tusiyoyafanya, na ambayo tungepashwa kufanya, Inategemea kanuni ya «sababu na matokeo yake» inayoitwa pia «kanuni ya panda na vuna».

Mambo inayounda mwenendo wetu inatujulisha sababu za «woga». Mambo hayo ndiyo inatenda kazi ndani ya hisia, hisi, mawazo, maneno na matendo yetu au tena ndani ya uongozi wa dhamiri yetu na pia ndani ya utendaji wa mfumo wetu wa neva. Mara nyingi, sababu hizo hatuzielezi kwetu wala kwa wengine

Sharti lingelikuwa tu tendo la kuamini, Mungu hangetutolea Amri kumi kupitia Musa, wala kupitia Yesu, mafundisho inayofungulia Mbingu mtu anayeyatekeleza. Sharti lingekuwa tu tendo la kuamini, Wamilele angelitutolea shauri hii: Furahieni tu kuamini! Endeleeni kubaki vipofu!

Mauti ni neno linalopinga uzima.

Misukumo chanya ya Mungu, sauti ya dhamiri yetu, hutufikia kupitia nafsi yetu. Roho wa Mungu anayetuhimiza, anayebisha mlangoni mwa dhamiri yetu, ni Roho wa milele ambaye ni uzima wa milele.

Hivyo, tukisikiliza Roho wa Mungu, dhamiri safi, atatuongoza maskani kwetu, kwa Mungu mweza yote, kwenye uzima safi wa kiroho tulimotoka na ambamo tutaishi tena milele. Kwa kuenda huko, njia ya nafsi hupitia «ahera» na mahali pa utakaso.

Mtu anayejifunza kusikiliza, na kuhisi mashauri ya dhamiri yake, anayeyatekeleza kusudi atende vema, mtu huyu hatua kwa hatua anajiokoa na woga. Anajihisi huru na mwenye kubebwa na nguvu chanya inayomletea salama na msaada toka moyoni mwake na kumfanya mwenye raha. Ni Chemchem asilia, yaani Mungu.

Kila moja ya maisha yetu mengi duniani ni zawadi kubwa ya nehema, ya upendo na ya huduma usio na mwisho wa Wamilele kwa wanae. Maisha duniani ni shule ambapo mtu ana wajibu wa kujifunza kutambua Uzima ni nini

Ukitenda kufuatana na maelekezo mema ya dhamiri yako, na ukiishi ukitekeleza mafundisho halisi ya Yesu, utaushika mkono wa Kristu, Yeye aliye na nuru yake, upendo wake na hekima yake karibu nawe. Hivyo, nguvu za Uzima, zenye nuru na nzuri, zitakuongoza daima siku zote na utakuwa basi katika hali nzuri.

Mtu anayekubali kujiswali, kujifunza kujitambua na anayekuwa na dhamiri ya hali zake mbovu kupitia matokeo ya maisha yake ya siku zote, atakuwa mshindi. Hatahofu kutafakari dhambi na makosa yake. Atajua kuvichanganua waziwazi, na kutoa somo kukupitia makosa hayo kwa ajili ya kuendelea kusonga mbele. Hali

hiyo ya uelekevu humletea mtu utulivu wa dhamiri, usalama,amani na hali shwari moyoni.

Kanisa hutumia neno mauti kama kitisho kwa lengo la kupokonya pesa mifukoni mwa waumini wanaongoja kifo, hadi muda watapovikwa sanda , ijapokuwa maishani mwao, kanisa liliwafanya waishi jehenamu, likiwashikilia katika ujinga, wakiwa wenye kujutia makosa yao, wenye hofu kubwa na wasio na matumaini.

Ni vema tuwe na dhamiri kwamba hakuna mtu aliye na uwezo wa kukabidhi mwenziwe au dini ya nje uzima wake wa duniani. Kila mtu anaalikwa na Roho mkuu kujitakasa, na kutakasa tabia yake. Kwa kufikia hayo, tufuate hekima ya Mungu katika Amri zake na mafundisho ya mlimani ya Yesu, Kristu. Isitoshe, leo tena, tumetolewa mafundisho tofauti ya kimungu yenye thamani kubwa inayoweza kutumiwa katika maisha ya kila siku, inayorudiliwa

tena na nguvu nyingi za kiroho na ambayo watu wote wanaweza kupata.

Marudio ya uzima wa dunia inamwezesha mtu kurekebisha, kukosoa dhambi alizozitenda muda wa maisha yake mengi ya awali duniani.

Kumbukumbu ya umwilisho wa awali ikifutwa, kila uzima duniani hugeuka mpya.

Katika Mungu, Muumba wa milele wa kile kisicho na mwisho, mnatawala mageuzi na mabadiliko, bali si uharibifu.

Hakuna kitu kimoja kilicho kufa kati ya vile vinavyoishi ndani ya kile kisicho na mwisho,kwa kuwa vyote ni nguvu, na nguvu ni uzima. Uzima unatiririka ahera na hata pia duniani humu.

Mto wa uzima wa ulimwenguni pote, unaoitwa pia nguvu ya ulimwenguni pote au uzima, unatiririka bila kukoma. Kwa hiyo, uzima hupo daima. Uzima ni nguvu, nguvu kuu tendaji. Mifumo yote ya uzima hutokana na nguvu hiyo.

Mkondo wa Uzima tunaouita pumzi yetu, nao pia ni nguvu ya ulimwenguni pote.

Kupitia pumzi yetu tumeunganishwa na ulimwengu, na mkondo wa ulimwenguni pote wa Uzima.

Chote kitokacho kwa Mungu – kwa mfano pumzi yetu, ambayo ni uzima wa nafsi na ganda la kufa la mwanadamu – hurudi ndani ya Roho, ndani ya Uzima. Mtu anapokufa, Roho, Uzima ulio ndani ya nafsi, huchukua, kupitia nafsi, pumzi iliyokuwemo ndani ya mtu na kuipulizia tena ndani ya nafsi kwa mwendo tofauti. Hivyo, kwa muda ule ule baada ya mtu kutoa pumzi yake ya

mwisho, nafsi, nayo, huvuta pumzi yake ya kwanza na kuanza kupumua kwa mwendo mwingine.

Namna yetu ya kufikiri na ya kuenenda husababisha mabadiliko ya ndani iletayo utakaso na kuangaziwa kwa nafsi na mwili au, tofauti na hayo, giza ya nafsi na mwili inayoambatana na mtetemo wa chini.

Kituo cha nafsi hupatikana kando ya ipofizia. Kama tulivyoeleza tayari, mwili wa asili ya nuru wa viumbe safi vya kiroho, kwa mfano nafsi, kiumbe cha kiroho, unaundwa na chembe za kiroho.

Maganda ya nafsi ni dhamiri ya mtu, inapatikana mwilini mwa mtu ndani ya «vituo vya dhamiri» vinavyofuatana kwenye uti wa mgongo. Maganda ya nafsi, au vituo vya dhamiri, inajaza kila seli na

kila kitu cha mwilini na nuru yao. Kiwango cha dhamiri cha mtu hulingana na kiwango cha nuru ya nafsini mwake. Jumla ya nuru inaunda haiba ya mwanadamu.

Nuru hizo zenye viwango tofauti vya kung'aa na mifuko ya nguvu ya nafsi mwilini ni kama pia kamba inayowasilisha, kurekodi na kuhifadhi ujumbe kati ya mtu, nafsi na vikundi vya sayari za maada safi za enzi za nafsi, ambamo mnahifadhiwa mambo iliyorekodiwa kuhusu mtu yule. Waya huo wa mawasiliano au wa ujumbe unaitwa tena kamba ya fedha au kitovu cha kiroho. Tunaweza kuuita pia kiwasilishi cha maumivu.

Hivyo, muda wa upasuaji au uchunguzi wa maiti au tena wa utoaji wa viungo, kwa mfano, mtu huyo anaweza kuhisi uchungu unaosababishwa na upasuaji huo wa mwili kupitia waya wa ujumbe, kiwasilishi cha uchungu. Basi, uchungu ambao mtu anahisi ni mkali mno.

Tunafahamu kwamba, kwa mjibu wa taratibu za kiganga na za upasuaji, ni lazima kiungo kilichokatwa kichungwe hai kusudi kiwe na uwezekano wa kupandikizwa. Ndiyo sababu mwili wa «mfu» aliye nusu «hai», anayeitwa « mtoaji wa kiungo», huifadhiwa na mashine. Hali hiyo ngumu ndio ukweli wa mambo nao humsababishia mtu huyo uchungu mkali mno.

Nafsi inapoingia katika mwili mpya hapa duniani, inakuja na mpangilio wa muda wake wa maisha ya kimwili. Muda huo huanzia tangu kuzaliwa na kuhitimishwa na kifo ambacho pia ni mauti.

Nafsi inatambua uhusiano wake na watu, inatambua mabaya iliyowatendea na jinsi watu hao walivyomtendea. Nafsi huhisi basi mwilini mwake uchungu au shida, kwa kifupi, yote aliyowatendea wenziwe, hata pia wanyama na mazingira. Kutambua

mwenyewe ubaya aliowatendea watu inawezesha nafsi kukiri uovu uliorekodiwa ndani ya mwili wake wa kiroho au ndani ya hali zilizo ndani ya maganda ya nafsi. Kufuatana na uovu, inawezekana pia kwamba ndani ya maganda ya nafsi mrekodiwe uwezo wa kurudilia upya maisha ya duniani unaoiwezesha kutubu na kurekebisha dhambi inazobeba na zilizo sasa picha halisi ya utu wake.

Inawezekana kwa nafsi katika miaka michache ya maisha ya kibinadamu kujikomboa toka mizigo fulani ya dhambi, ila nafsi inaweza kutumia pia vibaya umwilisho huo na kujiongezea tena mzigo wa dhambi. Ndiyo sababu, katika enzi za nafsi, kwa msaada wa malaika mlinzi wake au wa malaika mwalimu, nafsi ina uwezo wa kutathmini manufaa na ubaya wa umwilisho unaotazamiwa. Malaika huyo anamtolea maelekezo muhimu kuhusu lengo la uzima wa duniani, kuhusu wajibu wake. Hivyo nafsi inaweza kuamua kwa hiari yote. Hakuna nafsi inayoingia ndani ya

mwili mpya bila kufunzwa kwa namna hiyo. Kwa hiyo ina uhuru wa kukubali au kukataa maelekezo hayo.

Kufa na kuendelea kuishi kwa hali nyingine ni sehemu ya uzima wa dunia hii.

Uzima wa duniani ni wa thamani kubwa. Ni vema tuwe na dhamiri kwamba kila mwenendo mbaya una kinyume chake ambacho ni maadili na nguvu chanya ambazo tunaweza kukuza tukiupa wema thamani na kuutenda. Ni sisi. wenyewe tunaochagua ni nguvu ipi tuamshe.

Hali yote maututi ni aina ya vita kati ya mtu na nafsi yake. Anataka kulinda «Uzima» japo uzima huo umo ndani ya nafsi – ni uzima wa nafsi isiyokufa inayochukua sasa Uzima au pumzi.

Muda wa kifo, watu waliokuwa na dhamiri safi huona daraja la nuru likijengwa ndani mwao na inayowaletea hamu ya kuvuka daraja hilo.

Nafsi iliyojitenga kabisa na mwili wake wa kufa ina maada nyingine. Hali na umbo lake vinafana na umbo la mwanadamu ila maada na muundo wake ni laini na mwepesi sana.

Nyakati zinazofuata kifo cha mwili, nafsi hubaki mara nyingi kando ya mwili uliokufa. Nafsi inaweza kuumulikia mwili na nuru yake, inaweza tena kujipenyeza kwenye mwili ikiwa ungali bado joto, ila haiwezi tena kuurudishia uhai, au kutenda kazi ndani ya maada hiyo iliyokufa na nzito.

Baada ya kutoka mwilini, nafsi inaona ndani ya maganda yake mojawapo ya ndugu zake waliofariki. Inawaona na umbo lao la awali la kidunia na kutokana na uhusiano waliokuwa nao, hawa humsalimu

na kumtakia ujio mwema katika dunia hiyo ya wafu.

Ni uzito wa dhambi za nafsi au, kinyume na hayo, kiwango cha nuru yake ndivyo vinaonyesha aina ya uzima wa nafsi hiyo baada ya uzima wa dunia hii.

Tufahamu kwamba «mbingu» na «jehanamu» ni hali za dhamiri tunazounda sisi wenyewe.

Nafsi zinazoshikiliwa na dunia hubaki muda mrefu baina ya watu. Zinaambata wamoja, zinawatawala na kuwashawishi watende maovu. Kwa hiyo, nafsi hizo zinawasukuma, na kuwatumia na tena kuwaongoza watu hao kwa kutumia hali zao mbovu zote.

Ni vema tusisahau kwamba yote yanayotufikia, mazuri kama vile mabaya, yanaweza kuwa kitu chema kwa jambo fulani na kuwa na manufaa kwetu, ikiwa

tumejifunza kuona mazuri ndani ya kila jambo na kuyasisitiza ili kurekebisha yaliyo mabaya. Kwa kutenda kwa hali nzuri, tunajenga na kusisitiza nguvu nzuri ndani mwetu. Tendo hilo ni msaada na tena suluhisho inayotuwezasha kuishi vema na kuepuka mauti ya kiroho.

Mtu anayetenda kwa hekima ni yule anayetumia muda alioupewa duniani kwa kugundua kitu cha thamani kubwa au hazina ya kiroho na anayeizididisha kwa kutenda vema awezavyo. Anatoa yanayotoka kwa Mungu, akilenga furaha ya moyoni. Mtu anayegundua hazina halisi ya Uzima anaihifadhi muda wa maisha yake duniani na baada ya kifo. Mwisho wa uzima wa mtu huyo duniani, matendo yake huendelea kuishi ahera na nafsi yake inaingia ndani ya mazingira ya maisha iliyoangaziwa kwani matendo yake duniani ilikuwa mazuri.

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mafundisho ya Yesu Mlimani





Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake. *(Kurasa 48)*



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi, huhitaji mafunzo, kwa kuwa, sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu. *(Kurasa 56)*



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote. *(Kurasa 44)*

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
Gabriele-publishing.com



Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany
www.gabriele-publishing.com